

Maswali

1. Malaika aliambia yule mwanamke eti atakuwa na nini?
2. Vitu gani viwili vyenye malaika alimwambia huyo mwanamke kwamba mwanawe asifanye?
3. Mwanamke aliita mwanawe eti nani?
4. Mungu atafanya nini ikiwa Samsoni atamtii?
5. Mbona Samsoni alienda Timna?
6. Samsoni aliuuwa nini shambani?
7. Samsoni alipata nini kwa mzoga wa simba?
8. Samsoni alitega kitendawili eti nini kwa wageni wake wa arusi?
9. Samsoni alisema atawapa wageni nini ikiwa watategua kitendawili chake?
10. Wageni walipata jibu la kitendawili namna gani?
11. Samsoni alipata shuka na mavasi za kuwapa wageni namna gani?

Majibu

1. Malaika aliambia yule mwanamke kwamba atapata mwana.
2. Lazima asikunywe divai. Lazima asikate nywele.
3. Yule mwanamke aliita mwanawe Samsoni.
4. Mungu atamfanya Samsoni kuwa na nguvu sana.
5. Samsoni alienda Timna kuoa mwanamke Mfiliti.
6. Samsoni aliuuwa simba.
7. Samsoni alipata nyuki na asali kwenye mzoga wa simba.
8. Kutoka kwa mwenye kula kukatoka cha kukula. Kutoka kwa mwenye nguvu kukatoka kitamu.
9. Shuka 30 na mavasi 30
10. Wageni wa Samsoni waliambia mkewe awatafutie jibu.
11. Samsoni aliuuwa Wafilisti 30 na akachukua shuka na mavasi zao.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



21 Samsoni na simba

Marejeo

Waamuzi 14:5 - 19

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Samsoni alikuwa na imani kwa Mungu, na Mungu akamfanya kuwa na nguvu sana.

Maneno maalum

- 21.1 Malaika + mke + mwana + sinywe divai + sikate nywele + nguvu
- 21.2 Samsoni + pendwa + mke Mfiliti + oa + simba + nyuki + asali
- 21.3 Sherehe ya arusi + kitendawili + vifungu 30 vya nguo + shuka 30
- 21.4 Wageni wa arusi + hawakutegua kitendawili + mke wa Samsoni
+ udhika + siku ya 7 + akasema + simba + asali + wageni walifaulu
- 21.5 Samsoni + kasirika + ua Wafilisti 30

21.1 Kulikuwa na mwanamke aliyeishi Israeli lakini alikuwa na uchungu kwa sababu hakukuwa na watoto. Siku moja malaika akaja kumwona yeye na mmewe. Malaika alimwambia yule mwanamke kwamba atapata mwana. Huyu mwana hatakuwa wa kawaida. Malaika alimwambia kwamba huyo mwana lazima asikunywe divai yoyote tena lazima asikate nywele zake. Ikiwa atatii hizi amri, Mungu atamsaidia na atamfanya awe na nguvu sana na apige maadui wa Waisraeli.

Huyo mwanamke alifurahi sana aliposikia kwamba atapata mwana. Mwishowe alipata mwana na akamwita Samsoni. Muda wote Samsoni alikua, hakukunywa divai yoyote wala hakukata nywele zake. Mungu alimfanya kuwa wa nguvu sana.

21.2 Samsoni alipenda mwanamke Mfilisti aliyekaa Timna na alikuwa anataka amuo. Alipeleka baba yake na mama ili wamuone. Siku moja Samsoni alikuwa peke yake kwa shamba kule Timna na simba iliunguruma na kumwendea ili imshambulie. Lakini Samsoni hakuogopa kwa sababu alikuwa na nguvu na akiuwa kwa pigo moja.

Baada ya majuma machache Samsoni alienda Timna ili aoe mke aliyetaka na kuwa na sherehe ya arusi ya siku saba. Alipokuwa akipita kwa lile shamba, aliaamua kumwangukia yule simba aliyemuua. Aliona ndani ya simba, kundi kubwa ya nyuki na imetengeneza asali nyingi. Samsoni alichukua baadhi ya asali na akala. Alichukua hiyo asali na akampa baba yake na mama yake wakakula lakini hawakujua aliitoa wapi.



21.3 Kwa hiyo sherehe, Samsoni aliambia wageni wake, “Nina kitetawili na mkikitegua kabla ya sherehe iishe, nitampea shuka thelathini na vifungu thelathini vya nguo. Lakini msipotegua kitendawili, mtanipa shuka thelathini na vifungu thelathini vya nguo.”

Hiki ndiyo kitendawili chenye Samsoni aliwategea, “Kutoka kwa mwenye kula kukatoka chakula. Kutoka kwa mwenye nguvu kukatoka utamu.” Bahatisha kitendawili kina maana gani?

21.4 Wageni wa arusi walijaribu na kujaribu lakini hata baada ya siku tatu, hawakupata jibu. Kwa hivyo waliambia mke wa Samsoni awasaidie kupata jibu.

Aliuliza Samsoni amwambie lakini hakumwambia. Kwa hivyo alijifanya kukasirika sana na akasema, “Kama unanipenda ungeniambia.” Alikasirika sana mpaka siku ya saba akamwambia jibu. Haraka haraka akaenda kuambia wale wageni.

Samsoni alikuwa anazungumzia simba aliyemuua. Kutoka kwa mzoga wa simba (anayekula) Samsoni alipata cha kukula, na kutoka kwa simba aliye na nguvu kulitoka kitu kitamu – asali. Wageni waliambia Samsoni, “Nini kitamu kuliko asali, na nani wa nguvu kuliko simba?” Kwa hivyo walijishindia shuka thelathini na vifungu vya nguo.



21.5 Samsoni alikasirika sana kwa sababu wageni walitumia mkewe ajifanye amekasirika ili awambie. Alienda kwa mji wa Wafilisti kwenye adui wa Waisraeli waliishi na akaua watu thelathini yeye peke yake. Alichukua kutoka kwao shuka thelathini na vifungu thelathini vya nguo na akawapa wale watu walioteguo kitendawili.